Mafunzo ya Wasaidizi Ustawi Wa Jamii; Awamu Ya Pili:

Stadi za Kushughulikia watoto waishio katika mazingira hatarishi zaidi na Familia katika mazingira maalumu.

SIKU YA 3

Kupima mahitaji ya mtoto na familia kushughulikia mahitaji maalumu
Uwezo wa familia kukabiliana na hali kulingana na mazingira

Malengo

Kufikia mwisho wa somo hili wasaidizi Ustawi wa Jamii wataweza:

- Kutumia mchoro wa kiikolojia kama kitendea kazi kuwezesha kufanya upimaji ya watoto waliokatika mazingira hatarishi zaidi na familia kwa ufanisi zaidi.
- Kutambua mahitaji na mbinu zinazowezesha kufanya kazi na makundi yenye mahitaji maalumu, tofauti za kimila,wanawake,jinsia,yenye vurugu, Afya/ maswala ya afya ya akili. n.k.
- Kuelezea dhana ya familia kuwa na uwezo wa kukabiliana na hali kulingana na mazingira na jinsi tunavyoweza kuziimarisha familia, kwa kuzijengea uwezo ili ziweze kukabiliana na hali kulingana na mazingira tukiwa Wasaidizi Ustawi wa Jamii.

Upimaji

Rejea mafunzo yetu ya awamu ya kwanza

- Nini maana ya upimaji?
- Tunawezaje kufanya upimaji wa mahitaji ya mtoto na familia?
- Kwanini ni muhimu kumhusisha mtoto na familia kwa karibu katika kufaya upimaji?

Mchoro wa Kiikolojia: Kitendea Kazi Cha Msaidizi Ustawi Wa Jamii Katika Kufanya Upimaji

- Mchoro wa kiikolojia ni kitendea kazi kinacho muwezesha msaidizi ustawi wa jamii kupata uelewa mkubwa wa mtoto na familia yake
- Mchoro wa kiikolojia vilevile huonyesha uhusiano kati ya familia na rasilimali zinazomzunguka ikiwemo wanafamilia wengine na jamii
- Mchoro wa kiikolojia ni kitendea kazi kinachowezesha kupata taarifa zaidi kuhusu mahusiano ya kijamii kimuundokama tulivyojifunza katika mafunzo ya awali(PSWI)

Chanzo:Hartman, Ann. (1995). Diagrammatic assessment of family relationships. Families in Society: The Journal of Contemporary Social Services, 76(2) pp. 111-122.

Mchoro Wa Kiikolojia Kimuundo

Maeneo manne mbalimbali ya kukusanya taarifa kwa kina:

A. Taarifa kuhusu mtoto

B. Taarifa kuhusu Familia

C. Taarifa kuhusu wanafamilia wengine na Marafiki

A. Taarifa kuhusu Jamii

Hatua alipo Mtoto



Mchoro Wa Kiikolojia

- Ni kitendea kazi muhimu katika kufanya kazi na mtoto pamoja na familia katika kupimaji mahitaji yao.
- Mchoro huu ukamilishwe pamoja na mtoto na familia
- Ni muhimu katika upimaji, kupanga na kushughulikia mahitaji
- Huainisha hali halisi ya maisha ya familia kwa wakati
- Huonyesha mahusiano mazuri na vyanzo vya migogoro
- Huonyesha muelekeo wa rasilimali, au upungufu na kutopatiwa rasilimali
- Huonyesha maswala ya kufanyia kazi na rasilimali zinazohitajika.

Kanuni Za Msingi Kuhusu Mchoro Wa Kiikolojia

- ***Familia:*** Watu wote wenye uhusiano waishio ndani ya kaya, sehemu ya maelezo ya familia ni lazima ionyeshe umri na hali ya mwana familia ikiwa yu hai au amekufa.
- ***Ikolojia ya kijamii:*** Hali/sababu zote katika jamii zinazoweza kumuathiri mtu au watu katika familia. Sababu hizi za kiikolojiajamii hutofautiana kulingana na ukubwa au eneo kuashiria umuhimu wake.

Kanuni Za Msingi Kuhusu Mchoro Za Kiikolojia

- ***Viunganishi:*** muunganiko kati ya mtoto, familia, wanafamilia wengine na asasi za kijamii huonyeshwa kwa kutumia mistari. Mistari ya kuunganisha huweza kuwa minene kuashiria mahusiano yenye nguvu au myembamba kuashiria mahusiano dhaifu; mistari huelekea ndani au nje au pande zote.
- Kama zilivyo ramani zenye mambo mengi mchoro wa kiikolojia hubadilika kutegemeana na wakati na hupaswa kuchorwa tena pindi tukio muhimu linapotokea ndani ya familia.

Maelekezo Ya Kukamilisha Mchoro Wa Kiikolojia

- Ingiza majina ya wanakaya kwenye mduara mkubwa wa ndani
- Tumia mstatili kuonyesha jinsi ya kiume na mduara kuonyesha jinsi ya kike
- Ingiza umri kwa kila mmoja na tarehe/mwaka wa matukio ya maisha m.f. alipofariki
- Chora mstari ulionyooka unao unganisha mume na mke kuashiria ndoa
- Weka mkato kati ya mstari ikiwa wametalikiana
- Chora mstari unaoelekea chini toka kwa wazazi ili kuonyesha watoto walionao
- Chora mstari kuelekea juu kuonyesha babu na bibi
- Chora mduara au mstatili chini ya mduara wa familia kuashiria wanakaya wengine wasio na uhusiano na familia
- Weka alama ya × ndani ya mstatili au duara kuashiria kuwa muhusika amefariki

Maelekezo Ya Kukamilisha Mchoro Wa Kiikolojia

- Kisha onyesha mahusiano kati ya familia au mtu mmojammoja ndani ya familia na mazingira kwa kuchora mistari kati ya familia na mduara wenye mfumo husika.

Maelekezo Ya Kukamilisha Mchoro Wa Kiikolojia

- Aina ya mstari huashiria mahusiano yaliyopo
- Mstari mnene huashiria mahusiano yenye nguvu (mazuri)
- Mstari uliokatikakatika huashiria mahusiano dhaifu
- Mikato ndani ya mstari huashiria mahusiano yenye migogoro.
- Mishale iliyo katika mistari ya kuunganisna huonyesha muelekeo wa uwezo na rasilimali au .
- waulize wanafamilia kuhusu asili ya mahusiano waliyonayo na uandike maelezo mafupi kuhusu mistari husika kama ilivyoainishwa.



Mchoro wa Kiikolojia



Required

Maelekezo ya kukamilisha mchoro wa kiikolojia…

- Kisha ongeza mistari ya kuunganisha kati ya wanafamilia au mtu mmojammoja pamoja na mazingira kwa ujumla kwa kuchora mistari kati ya familia na mduara wenye mfumo husika.

Inahitajika

Mchoro wa kiikolojia unaoonyesha ndoa yenye ukewenza (wake wawili)



Inaonyesha kaya moja tu. Je kuwe na miduara tofauti kwa kuonyesha kaya tofauti?

Inahitajika



Need to modify with Tanzanian names and add grandparents

Majadiliano

- Je unawezaje kukitumia kitendea kazi hiki?
- Je unawezaje kuoanisha kitendea kazi hiki na dodoso la upimaji ya hali ya mtoto (CSI) na mpango wa huduma?
- Mawazo mengine?

Zoezi Katika Vikundi Vidogo– Kamilisha Mchoro Wa Kiikolojia

- Gawanyikeni katika vikundi vidogo vidogo
- Tumia mfano wa uzoefu toka kwa mmoja wa wana kikundi, fanyeni igizo dhima likionyesha jinsi msaidizi ustawi wa jamii anavyofanya mahojiano na wanafamilia ili kupimaji mahitaji ya mtoto.
- Kamilisha mchoro wa kiikolojia kulingana na upimaji yako

Zoezi Katika Vikundi Vidogo– Kamilisha Mchoro Wa Kiikolojia

- Mrejesho wa kazi ya vikundi
- Je tumejifunza nini?

Kamilisha Mchoro Wa Kiikolojia

- ***Mapendekezo:*** Kamilisha mchoro wa kiikolojia kwa familia yako binafsi na uwe makini katika hisia zinazoambatana na zoezi hili, pamoja na udhaifu katika mahusiano na wengine.

  Inawezekana kukawa na taarifa mpya au mapungufu katika taarifa. Tutajadili pamoja na kundi wakati wa uwasilishaji katika kundi kubwa.

Mahitaji Maalumu Kulingana Na Utofauti Wa Mila Na Hali Ya Familia

Je ni tofauti gani za mila na hali ya familia unazokabiliana nazo?

Bungua bongo

Mahitaji Maalumu Kulingana Na Utofauti Wa Mila Na Hali Za Familia

- Ni tofauti gani za hali ya familia ulizowahi kukabiliana nazo?
- Ndoa za uke wenza.
- Vipengele mbalimbali vya mila
- Wafugaji au familia zinazo hamahama
- Wengineo?
- Ni ipi baadhi ya mikakati ya kushughulikia mahitaji yao?

Mahitaji Maalumu Kulingana Na Utofauti Wa mila Na Hali Za Familia

Wasaidizi ustawi wa jamii wanapaswa:

•Kuwa na ufahamu kuhusu mila za familia husika (Ujuzi mbalimbali)

•Kujenga stadi zinazooana na ujuzi wa mila m.f. mahusiano ya unasihi katika kufanyakazi na familia pamoja na mifumo ya kimila.

Mahitaji Maalumu Kulingana Na Utofauti Wa Mila Na Hali Za Familia

Wasaidizi Ustawi wa Jamii wanapaswa:

- kutumia njia ya maswali yaliyo wazi na kuachilia mbali uelewa wake wa awali kuhusu mila na desturi za mteja aliyenaye
- kusikiliza uzoefu wa mteja uliyenaye

Mifano ya Visa-mkasa

- Salama ni msichana wa miaka 13 ambae hufanya kazi ya biashara ya ukahaba . Anamatatizo ya kutosikia vizuri na anatoa taarifa kuwa baadhi ya wateja wake wamekuwa na vurugu(wakitumia nguvu)
- Zena ni mwanamke mwenye miaka 36 amekuwa kipofu kwa maisha yake yote . Anao watoto watatu, kati yao mmoja ni mvulana mwenye umri wa miaka 12 , alianza shule akiwa mdogo sana na sasa yuko mtaani na anafanya biashara ndogondogo za kuuza maji, mayai, na vitu vingine ili kusaidia familia kiuchumi. Anae binti wa miaka 7, ambaye hataki kwenda shule pamoja na mtoto wa kiume wa mwaka mmoja anayehitaji malezi ya karibu
- Adam ni mvulana kati ya watoto 12 kwenye familia ya ukewenza ya mzee Mwakipesile. Anahisi kama hakuna anayemjali, baba yake humpendelea mtoto wa rika lake aliyezaliwa na mke mdogo . Adam amekuwa na vurugu na hugombana na watoto wengine.
- Happiness ni mwanamke mwenye umri wa miaka 27 . Ana mtoto mmoja mwenye miaka 4 . Alipokuwa mjamzito alifanyiwa uchunguzi wa damu na kugundulika kuwa ana Virusi Vya UKIMWI. Mume wake alimuacha kwa kumtuhumu kuwa ameleta maambukizi ya VVU katika familia. Ni mwenye ghadhabu na huzuni na hayuko tayari kuanza kumeza dawa za kufubaza VVU .

Je Wana Mahitaji Gani Maalumu?

- Salama
- Zena na watoto wake
- Adam
- Happiness

Kushughulikia Mahitaji Maalumu

- Mshughulikie mteja kwa ujumla wake
- maswala ya kimila yanaweza kujumuishwa na matatizo mengine kwa ujumla
- Unapaswa kumsaidia mteja aelewe kuwa matatizo mbalimbali huambatana na tunapaswa kushughulikia tatizo moja kwa wakati kulingana na uhitaji.
- mteja anaweza kuunganishwa na watu wengine wenye matatizo mengi mchanganyiko kama yake.

Masuala Yanayohusu Wanawake

- Ushirikishwaji kamili wa wanawake katika kufanya maamuzi kuhusu mambo yanayowahusu pamoja na maswala ya sera.
- Wanawake wengi hutanguliza mahitaji ya watoto wao kabla ya mahitaji yao kwanza.
- maswala ya wanawake kuwa na udhibiti kuhusu ngono salama na kuzuia maambukizi.
- Mengineyo???

Jukumu la msaidizi Ustawi wa Jamii: Kumtia moyo mwanamke kushirikishwa katika kushughulikia maswala ya kutokuwepo na usawa, kusaidia katika kupanga mipango na kutatua matatizo

Masuala Yanayohusu Mahusiano

- Kuheshimiana kulingana na wadhifa wa mtu
- Mahusiano yenye kusaidiana katika misingi ya kuaminiana
- Kushirikiana kwa pamoja
- Kushirikishana faida
- Majadiliano /mawasiliano
- Kushirikiana katika matatizo na kuwa sehemu ya suluhisho

Jukumu la Msaidizi Ustawi wa Jamii: Kuwa msikivu, tambua tatizo, Wasaidie wenza kupanga mpango. Toa rufaa kwa unasihi wa kitaalamu ikiwa utahitajika

Masuala Yanayohusu Matatizo Mbalimbali Ya Kiafya

- Pata ugunduzi kamili wa tatizo ikiwemo VVU na matatizo mengine ya kiafya.
- Pata huduma na ushirikiane na watoa huduma wengine
- Je kuna maswala ya kimila na kiuchumi yanayoathiri jinsi ya kushughulikia magonjwa?

Jukumu la Msaidizi Ustawi wa Jamii: Toa taarifa, saidia kutatua migogoro, fanya utetezi na uwe kiungo kati ya mteja na watoa huduma za afya

Masuala Yanayohusu Vurugu

- Elewa jinsi mtazamo wa jamii kuhusu jinsia unavyosababisha vurugu dhidi ya wanawake
- Wajumuishe wanawake na wanaume kwa usawa katika kufanya maamuzi na kuwa na amani.
- Vurugu zina athari zinazoendelea katika mfumo wa familia .
- Upatikanaji wa rasilimali ili kushughulikia maswala ya vurugu, kwa kuzingatia unyeti wa mila.

Jukumu la msaidizi Ustawi: Jielimishe mwenyewe pamoja na wateja, kutatua matatizo, rufaa kwa rasilimali husika, Fuatilia na fanya uteteazi

Masuala Yanayohusu Jinsia, Ujinsia Na VVU

- Wanawake wanahitaji ushirikiano wa wanaume ili waweze kujikinga
- Mahali ambapo kondom ndio njia kuu ya kujikinga, wanawake hutegemea wenza wao wawe waaminifu
- Tabia za wanaume huwaweka wanawake katika hatari ya maambukizi ya VVU.
- Kuwajengea uwezo kunapaswa ushughulikie suala la muundo wa kijamii uliopo ,asasi na mahusiano ambayo ndio msingi wa kutokuwa na uwiano

Jukumu la msaidizi Ustawi: kuwajengea uwezo wanawake, kushughulikia maswala ya kijamii na kimila , saidia kushirikisha wadau wote katika kufanya maamuzi, kutatua matatizo, au fanya igizo dhima kuonyesha jinsi ya kujenga uwezo kwa wanawake

Masuala Yanayohusu Utumiaji Wa Madawa Mengine

- Pombe, Bangi na “dawa za kulevya” huweza kuwa sababu Zinazochangia maambukizi ya VVU, uzingatiaji na hali bora ya maisha kwa watu waishio na VVU.
- Pombe na dawa zingine huweza kuathiri maamuzi kuhusu tabia hatarishi
- Programu za tiba dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya na vikundi vya msaada vinapatikana nchini Tanzania
- Utumiaji huu wa madawa huweza kuathiri msukumo wa damu, lishe pamoja na matatizo mengine.

Jukumu la msaidizi Ustawi: waelimishe watoto na familia kuhusu madhara ya utumiaji dawa, msaidie mteja kufanya mabadiliko kuhusu kutumia dawa . Kwa hatua hii msaidizi Ustawi anapaswa kutoa rufaa kwenda kwa watua huduma wegine kwa ajili ya tiba au msaada wa vikundi.

Kujenga Uwezo Wa Familia Kukabiliana Na Hali Kulingana Na Mazingira

Reference: Child Welfare Information Gateway, U.S. Dept. Health and Human Services, Admin. For Ch. And Families, Strengthening Families and Communities: 2011 Resource Guide, downloaded July 1, 2011 http://www.childwelfare.gov/preventing/promoting/protectfactors/.

Uwezo wa Kukabiliana Na Hali Kulingana Na Mazingira

Watoto Kwanza
Kuwalinda Watoto
Kuimarisha Familia

Muainisho Wa Mada

- Nini maana ya uwezo wa kukabiliana na hali kulingana na mazingira?
- Maeneo matano yanayoonyesha ushahidi wa uwezo wa kukabiliana na hali kulingana na mazingira katika kufanyakazi na familia
- Jinsi tunavyoweza kutumia uwezo huu tukiwa wasaidizi Ustawi wa Jamii.

Nini maana yauwezo wa kukabiliana na hali kulingana na mazingira?

Zipi ni sababu za ulinzi kwa mtoto na familia ambazo zinawawezesha kukabiliana na matatizo magumu na kuweza kurudia hali zao za kawaida?

Bungua bongo

Nini maana ya uwezo wa kukabiliana na hali kulingana na mazingira?

- Uwezo wa kukabiliana na hali kulingana na mazingira /Sababu za ulinzi ni hali ambayo kuwepo kwake katika familia au jamii huongeza afya na hali bora za watoto na familia.
- Sababu hizi au hali huimarisha uwezo wa familia kukabiliana na msongo . Ni kama kinga dhidi ya shinikizo, hupunguza madhara ya tatizo au msongo na husaidia mtoto pamoja na familia kutafuta msaada au mikakati ya kukabiliana inayoweza kuruhusu kufanya shughuli zao kwa ufanisi, hata katika hali ya kuwa na msongo. Sababu hizi husaidia wazazi na walezi kulea kwa ufanisi.

Maeneo Matano Yanayoonyesha Ushahidi Wa Uwezo Wa Kukabiliana Na Hali Kulingana Na Mazingira

Tafiti zimeonyesha kuwa uwezo wa kukabiliana na hali kulingana na mazingira/sababu za ulinzi zinahusishwa na matukio machache ya unyanyasaji na kutojaliwa:

- Malezi na upendo
- Ufahamu kuhusu malezi ya toto na maendeleo ya kijana
- Uwezo wa familia kukabiliana na hali kulingana na mazingira
- Mahusiano ya kijamii
- Msaada madhubuti kwa wazazi

Chanzo: Child Welfare Information Gateway, USHHS, ACF, July 1, 2011. http://www.childwelfare.gov/preventing/promoting/protectfactors/

1. Malezi na upendo

- Kama tulivyojadili katika mafunzo ya awamu ya kwanza (PSW I), uzoefu alioupata mtoto kuhusu malezi na kujenga uhusiano na mlezi (mtu mzima) unaathiri maeneo yote ya kitabia na maendeleo. Wazazi na watoto wanapokuwa na ushirikiano imara, kuna kuwa na hisia za upendo kati yao, Watoto hujenga imani kuwa wazazi wao watawapatia mahitaji yao ili kuishi, ikiwemo upendo, kukubali, malezi chanya na ulinzi.
- Tafitit zinaonyesha kuwa watoto wanaopokea upendo na malezi kutoka kwa wazazi wana nafasi nzuri zaidi ya maendeleo ya kiafya. Mahusiano ya mtoto na muendelezo wa malezi, Malezi ya mtumzima anayejali katika miaka ya mwanzoni inauhusiano wa maendeleo mazuri ya kitaaluma hapo baadae,tabia njema, mahusiano mazuri na wana rika na uwezo mkubwa wa kukabiliana na Msongo

1. Malezi na Upendo

- Kwahiyo malezi na upendo wa kutosha ni sababu za ulinzi zinazosaidia familia kukabiliana na hali kulingana na mazingira,au uwezo wa kuhimili hali ya msongo

2.Ufahamu kuhusu malezi ya mtoto na maendeleo ya kijana

- Kuna tafiti za kina zinazooanisha maendeleo mazuri ya afya ya mtoto na malezi yenye ufanisi mzuri. Watoto husitawi iwapo wazazi huwapa sio tu upendo bali pia hutumia mbinu nyingine a malezi yenye ufanisi yanayozingatia kanuni za malezi, ikiwemo mawasiliano yenye heshima na kusikiliza, kanuni zenye muendelezo ma matarajio na fursa salama zinazo endeleza uhuru.

2.Ufahamu kuhusu malezi ya mtoto na maendeleo ya kijana

- Malezi yenye mafanikio yanawezesha kurekebika kisaikolojia, huwezesha mtoto kuwa na mafanikio ya kitaaluma shuleni, huhamasisha udadisi kuhusu ulimwengu, na huhamasisha watoto kufikia malengo.
- Hivyo ufahamu na matumizi ya mbinu za malezi yenye ufanisi ni sababu ya ulinzi inayosaidia familia kuwa na uwezo wa kukabiliana na hali kulingana na mazingira au uwezo wa kuzuia hali ya msongo.

3. Malezi yanayo kabiliana na hali kulingana na mazingira

- Wazazi au walezi wengine wanaoweza kukabiliana na msongo wa maisha ya kilasiku, pamoja na dharura, kuwa na uwezo wa kukabiliana na hali kulingana na mazingira wao wenyewe ; wanao utayari wa kubadilika kulingana na hali na uwezo wa ndani unao wezesha kuhimili mambo yanapokwenda isivyotarajiwa
- Mambo mengi yanayosababisha msongo wa maisha, kama vile historia ya unyanyasaji ndani ya familia au kutojaliwa, matatizo ya kiafya ,migogoro katika ndoa, au vurugu za majumbani au jamii na msongo wa kiuchumi kama vile kukosekana kwa ajira, umaskini na kutokuwa na makazi hupunguza uwezo wa familia kukabili kwa ufanisi msongo wa siku hadi siku katika malezi ya watoto.

3.Uwezo wa wazazi kukabiliaana na hali kulingana na mazingira

- Kwahiyo msaada wa kuimarisha uwezo wa wazazi na walezi kukabiliana na hali ya shinikizo ni jambo linalochukuwa nafasi ya kuwa na uwezo wa kuisaidia familia kufikia uwezo wa kukabiliana na hali kulingana na mazingira, au uwezo wa kuzuia hali ya shinikizo.

4. Mahusiano ya kijamii

- Wazazi au walezi wengine wenye mtandao wa kijamii unaotoa msaada wa kihisia kwa marafiki, familia, na majirani mara nyingi hutambua kwamba ni rahisi kulea watoto wao na wao wenyewe. Wazazi wengi huhitaji watu wanaoweza kuwasiliana nao pindi wanapohitaji msikilizaji anayeweza kusikitika pamoja nao, kushauri, au msaada madhubuti
- Tafiti zimeonyesha kuwa wazazi waliotengwa, na mahusiano ya kijamii, wako katika hatari kubwa ya unyanyasaji wa watoto na kutojaliwa.

4. Mahusiano ya kijamii

- Hivyo msaada katika kuimarisha uwezo wa mzazi au mlezi na msaada wa mtandao wa kijamii ni sababu ya ulinzi inayoweza kusaidia familia kufikia hali ya kuweza kukabiliana na hali kulingana a mazingira

5.Msaada madhubuti kwa wazazi na walezi wengine

- Sababu nyingi tofauti huathiri uwezo wa familia kulea watoto wao. Familia zinazoweza kujipatia mahitaji yake ya msingi yenyewe kama chakula, mavazi, makazi na usafiri- na nani anafahamu namna ya kuzifikia huduma muhimu kama vile malezi ya watoto, huduma za afya, na huduma za afya ya akili kushughulikia mahitaji maalumu ya familia—zinaweza vizuri zaidi kuhakikisha usalama na hali bora ya watoto wao
- Kufanyakazi na wazazi kutambua na kuzifikia rasilimali katika jamii zinazoweza kuzuia msongo ambao mara nyingine huchangia kutokutendewa haki mtoto. Kutoa msaada madhubuti huweza pia kusaidia kuzuia kutojaliwa kusikokusudiwa ambapo mara nyingine hutokea wakati wazazi wanaposhindwa kuwahudumia watoto wao

5.Msaada madhubuti kwa wazazi na walezi wengine

- Tafiti zimeonyesha kwamba kuhakikisha kuwa familia zinapata mahitaji yao ya msingi ni sababu ya ulinzi inayosaidia familia kuwa na uwezo wa kukabiliana na hali kulingana na mazingira.

Ni njia gani ambazo wasaidizi ustawi wanaweza kusaidia kuwa na uwezo wa kukabiliana na hali kulingana na mazingira/Sababu za ulinzi kwa watoto walio katika mazingira hatarishi na familia zao?

Bungua bongo

Ni njia gani ambazo wasaidizi ustawi wanaweza kusaidia kuwa na uwezo wa kukabiliana na hali kulingana na mazingira/Sababu za ulinzi kwa watoto walio katika mazingira hatarishi na familia zao?

Tafiti zimegundua kwamba ifuatayo ni mikakati madhubuti ambayo msaada wa familia na programu za kuzuia unyanyasaji wa mtoto zinaweza kutumia kuendeleza sababu hizi za ulinzi

Ni jinsi gani wasaidizi ustawi wa jamii wanaweza kuwawezesha wanafamilia na watoto waishio katika mazingira Hatarishi kuwa na uwezo wa kukabiliana na hali kulingana na mazingira/Kuwa na sababu za ulinzi.

- ***Wezesha mahusiano kirafiki na kusaidiana.*** Kutoa fursa kwa wazazi na walezi wengine majirani kufahamiana, Kujenga mfumo wa ushirikiano, na kuchukua jukumu la kuongoza.Mikakati inaweza kujumuisha shughuli za kijamii, Kushirikiana chakula,Madaraja, mpangilio wa rasilimali au mitandao ya kijamii itakayowezesha mifumo ya kusaidiana kati ya familia zenye uhitaji. Wanafamilia wanaweza kuhusishwa katika uongozi wa shughuli hizi pamoja na fursa nyingine za kujitolea.

Ni njia gani ambazo wasaidizi ustawi wanaweza kusaidia kuwa na uwezo wa kukabiliana na hali kulingana na mazingira/Sababu za ulinzi kwa watoto walio katika mazingira hatarishi na familia zao?

- ***Kuimarisha malezi.*** Kubuni njia ambazo wazazi na walezi wengine watapata msaada wa maswala ya malezi wanapohitaji. Uwezekano ni pamoja na madaraja, vikundi vya msaada, kutembelea majumbani, na taarifa zilizo kwenye maandishi.
- ***Kushughulikia dharura za familia.*** Toa msaada wa ziada kwa familia nyakati za dharura au matatizo mengine magumu. Mfano mwanafamilia anapougua, wakati wa ukame au mavuno hafifu, kupotelewa kwa nyumba au matatizo mengine.

Ni njia gani ambazo wasaidizi ustawi wanaweza kusaidia kuwa na uwezo wa kukabiliana na hali kulingana na mazingira/Sababu za ulinzi kwa watoto walio katika mazingira hatarishi na familia zao?

- ***Kuziunganisha familia na huduma pamoja na fursa nyinginezo.*** Toa rufaa kujenga stadi mpya ,elimu, huduma za afya, unasihi na misaada mingine toka kwa wahuduma ndani ya jamii.
- ***Thamini na wasaidie wazazi na walezi wengine*****.** Mahusiano kati ya familia na watoa huduma ni muhimu …hutoa msaada wa kisaikolojia na hutambua utayari wa walezi watoto hawa, husaidia familia kushughulikia hali ngumu.

Ni njia gani ambazo wasaidizi ustawi wanaweza kusaidia kuwa na uwezo wa kukabiliana na hali kulingana na mazingira/Sababu za ulinzi kwa watoto walio katika mazingira hatarishi na familia zao?

- ***Wezesha maendeleo ya mtoto kijamii na kihisia***

  Msaidizi ustawi anaweza kutoa msaada wa awali wa kisaikolojia au kuainisha watu wengine wanaoweza kutoa unasihi kwa watoto au msaada kuwezesha maendeleo yao ya kijamii na kihisia. Wakati watoto wanapoleta nyumbani yale waliyojifunza, wazazi hufaidika vilevile.
- ***Angalia na ufanyie kazi viashiria vya awali vya hatari vya unyanyasaji wa mtoto au kutojaliwa.*** Msaidizi ustawi anapaswa kumuangalia mtoto anayemhudumia kwa uangalifu na ashughulikie mara aonapo daliliya tatizo lolote. Kushughulikia tatizo mapema husaidia kuhakikisha usalama wa mtoto na mzazi kupata msaada na huduma wanayohitaji. Msaidizi ustawi anaweza kuelimisha walezi kugundua dalili za unyanyasaji na kutojaliwa toka kwa watu wazima.

Muhtasari Na Mrejesho Kwa Siku Ya Kwanza

Mrejesho katika kundi kubwa na kupongezana